



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 02/11/2023

TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA KWA AJILI YA UJENZI WA MIUNDO MBINU YA VYOO NA MFUMO WA KUNAWIA MIKONO SHULE ZA MSINGI BUNYANGOMALE NA IBUKA.

ZABUNI NA: LGA/071/2023/2024/RDC/W/19 – LOT 01

1. **Mkurugenzi Mtendaji (W)** anawatangazia Wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa Miundo Mbinu ya Vyoo pamoja na Mfumo wa Kunawia Mikono shule za Msingi Bunyangomale na Ibuka. itakayojengwa katika Kata ya Masoko na Masebe kupitia **Programu ya Mradi wa SWASH** kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
2. Ujenzi wa Miundo mbinu katika Shule hizo utahusisha ujenzi wa **Miundo mbinu ya vyoo, mfumo wa kunawia Mikono pamoja na uvunaji wa maji.**
3. Hivyo basi, Mkurugenzi Mtendaji (W) anakaribisha Mafundi ujenzi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kuomba kazi za Ufundi kwa utaratibu wa **"Force Account"** katika fani na sifa za Ufundi zifuatazo:-
4. Ujenzi wa **Miundo mbinu ya Shule** inatarajiwa kujengwa katika shule za Msingi kwa mchanganuo ufuatao:-

Zabuni Na.	KITALU (LOT) NA.	JINA LA SHULE YA MSINGI	MIUNDO MBINU
LGA/071/2023/2024/RDC/W/19 – LOT 01	1	Bunyangomale	Miundo mbinu ya maji safi na Maji Taka
	2	Ibuka	Miundo mbinu ya maji safi na Maji Taka

Hivyo basi, Mkurugenzi Mtendaji (W) anakaribisha Mafundi ujenzi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kuomba kazi za Ufundi kwa utaratibu wa "**Force Account**" katika fani na sifa za Ufundi zifuatazo:-

i. Fundi Uashi (Ujenzi wa Msingi, Kuta na Rinta),

- Awe na elimu ya ufundi Uashi/ujenzi na mwenye kujua kusoma ramani za majengo.
- Awe na vitendea kazi za kunyoosha ukuta kama vile Square, bridge (Plumb Bob), mwiko, Komabao, Pima maji n.k
- Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani
- Awe na uwezo wa kupaua majengo ya Serikali kwa kutumia mbao laini.
- Awe na uwezo wa kupiga dari (brundering) na kufunga Gypsum
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni

ii Fundi Seremala (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za Milango

- Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya mbao ngumu
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni..

9. Pamoja na sifa zilizotolewa hapo juu waombaji wanapaswa kuzingatia masharti kama ifuatavyo:-

- Awe Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
- Awe na Namba ya Utambulisho wa mlipa kodi (TIN) (aambatanishe na barua ya maombi kwa uthibitisho zaidi)
- Awe na akaunti ya benki kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe.
- Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Mtaa anakoishi.
- Awe tayari kufanya kazi muda wote hadi mradi utakapokamilika


10. Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu ziwasilishwe ofisi ya Mwalimu Mkuu, **Shule ya Msingi Bunyangomale na Ibuka, S.L.P 148, Tukuyu** yakiwa yamefungwa kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi ya Ufundi unaoombwa mfano **Ufundi Uashi n.k**

11. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi za ufundi ni siku ya Ijumaa ya Tarehe 08/11/2023 kabla ya saa 5:00 Asubuhi. Aidha, maombi yatakayoletwa baada ya

hapo hayatakubaliwa.

12. Waombaji wote wanatakiwa kuhudhuria usaili wa mafundi wa utakaofanyika tarehe 08/11/2023 saa 6:00 Mchana utakaambatana na kuwashindanisha nukuu za bei za ufundi.

13. Wako katika ujenzi wa Taifa



Mchau, R.B

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE**